

TAARIFA KWA UMMA



TANGAZO HILI LIMEIDHINISHWA NA MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (CMSA)

UTOAJI WA HISA ZA UPENDELEO 97,646,913 ZA BENKI YA DCB COMMERCIAL BANK (DCB)

DCB Commercial Bank PLC inatoa taarifa kwa umma kuwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Matarajio wa DCB Commercial Bank Plc kuuza hisa za upendeleo 97,646,913 kwa wanahisa wake kwa bei ya Shilingi 110 kwa kila Hisa.

TAARIFA YA UTOAJI WA HISA ZA UPENDELEO ZA DCB COMMERCIAL BANK:

Muhtasari wa taarifa muhimu kuhusu hisa za upendeleo za DCB Commercial Plc zimewekwa hapa chini:

Mtoaji:	DCB Commercial Bank PLC
Bei:	Shilingi 110 kwa kila hisa
Idadi ya hisa zinazotolewa:	Hisa 97,646,913
Mtaji uliokusudiwa kukusanywa:	Shilingi 10,741,160,430
Uwiano wa hisa za upendeleo:	Hisa 1 mpya kwa kila hisa 1 iliyopo

Uwekezaji unafanyika kwa njia ya Wanahisa kujaza fomu za maombi zitakazotumwa kwao. Wanahisa wanashauriwa kusoma waraka wa matarajio na fomu za maombi zitakazotumwa. Waraka wa matarajio unapatikana kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya DCB Commercial PLC www.dcb.co.tz na kupitia Mshauri Kiongozi (iTrust Finance Limited): Barua pepe: dcbrightsissue@itrust.co.tz Simu: +255 743 786 236.

Maombi yatakamilishwa kwa kufanya malipo katika akaunti ya DCB Commercial Bank iliyoorodheshwa hapa chini:

Akaunti ya Malipo

DCB RIGHTS ISSUE COLLECTION ACCOUNT	22100145
-------------------------------------	----------

TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU:

S/n	Tukio	Tarehe
1.	Tarehe ya mwisho kununua Hisa	Jumanne, 05 Novemba 2024
2.	Tarehe ya Rekodi	Ijumaa, 08 Novemba 2024
3.	Usambazaji wa Fomu kwa wanahisa	Jumatatu, 11 Novemba 2024
4.	Kufungua Mauzo ya Hisa za Upendeleo	Jumatatu, 11 Novemba 2024
5.	Kufunga Mauzo ya Hisa za Upendeleo	Ijumaa, 6 Desemba 2024
6.	Tangazo la matokeo ya Mauzo ya Hisa	Jumatano, 11 Desemba 2024
7.	Wasilisho la Rejesta kwa CSDR	Alhamis, 12 Desemba 2024
8.	Kuorodheshwa kwa Hisa DSE	Jumatano, 18 Desemba 2024

Wawekezaji wanashauriwa kuwasiliana na mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam wenye leseni kutoka Mamlaka ya Masoko, Mitaji na Dhamana (CMSA); wahasibu, wanasheria au washauri wengine wa masuala ya fedha kwa ushauri elekezi ili kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mtendaji,
DCB Commercial Bank PLC,
DCB House,
Magomeni Mwembechai,
Plot No. 183, Block R,
Morogoro Road, P.O. Box 19798,
Dar es Salaam, Tanzania.